JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA

ISSN 0856 - 4965 | TOLEO NO. 11 | APRILI - JUNI 2025

# JARIDA LA TAFORI



SCAN ME

FOR DIGITAL VERSION

**TAFORI YAFANIKISHA KONGAMANO LA TATU LA KIMATAIFA LA KISAYANSI**

**TAFORI YAANZISHA MASHIRIKIANO NA CHUO KIKUU CHA SAINT PETERSBURG STATE CHA URUSI**

**SIFA ZA ASALI YA TANZANIA ZAONESHA UPEKEE KATIKA SOKO LA KIMATAIFA**

JARIDA HILI HUTOLEWA NA KUSAMBAZWA NA TAFORI

@taforitz | www.tafori.or.tz





# UJUMBE KUTOKA KWA

## Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania | TAFORI

**Mpendwa Msomaji**

Napenda kuchukua nafasi hii kukukaribisha tena kwenye toleo letu la Juni 2025 la Jarida lako pendwa la Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI). Jarida hili huchapishwa mara nne kwa mwaka. Wachangiaji katika Jarida hili ni watafiti na wadau wengine wa misitu na nyuki ambao wanataarifa au makala muhimu kwa ajili ya kuelimisha jamii.

Toleo hili linakuletea taarifa mbalimbali zinazohusiana na utafiti wa misitu na nyuki lakini pia na Serikali ilivyojipanga kuimarisha uwezo wa TAFORI ili kutoa huduma bora na kuboresha utafiti wa rasilimali za misitu na nyuki. Miongoni mwa taarifa zilizomo ndani ya toleo hili ni namna TAFORI ilivyofanikisha Kongamano la Tatu la Kimataifa la Kisayansi lililofanyika Disemba 11 – 13, 2024 jijini Arusha, mashirikiano ya TAFORI na Chuo Kikuu cha Saint Petersburg State cha Urusi ikiwa ni njia mojawapo ya kuimarisha utafiti wa misitu na nyuki nchini pamoja na TAFORI inavyoendelea kuboresha miundombinu yake ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Nipende kutoa shukrani za pekee kwa waandishi wote walioandaa makala kwa ajili ya Jarida hili. Aidha shukrani ziwafikie pia wahariri wote kwa kazi yao nzuri ya kuhariri na kuhakiki makala za Jarida hili.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la TAFORI.



Dkt. Revocatus Mushumbusi

**MKURUGENZI MKUU**

**TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA (TAFORI)**



# YALIYOMO


Neno Kutoka kwa Mhariri Mkuu ..... 2

Uoteshaji wa Mianzi kwa Njia ya Vikonyo Yawa Chachu Katika Kilimo Kibiashara, Uhifadhi wa Mazingira ..... 4

Upimaji wa Ubora wa Mbao kwa Tensiomita ni Fursa kwa Wadau Wa Misitu ..... 6

Sifa za Asali ya Tanzania Zaonesha Upekee Katika Soko la Kimataifa ..... 8

Ufugaji wa Nyuki Wasiodunga Katika Maeneo ya Makazi ..... 10

TAFORI Yaboresha Mazingira ya Utendaji Kazi Kupitia Ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ..... 12

Tafiti za Udongo Zinavyowezesha Upandaji wa Miti Kwenye Maeneo Sahihi ..... 14

TANGAZO - Forestry Researchers Registration Application Form ..... 17

TAFORI Yafanikisha Kongamano la Tatu la Kimataifa la Kisayansi ..... 18

TAFORI Yaanzisha Mashirikiano na Chuo Kikuu cha Saint Petersburg State cha Urusi Katika Kuimarisha Utafiti wa Misitu na Nyuki Nchini ..... 22

TAFORI, WWF, MCDI Zaimarisha Umoja wa Vijiji Vyenye Hifadhi ya Misitu Kusini mwa Tanzania ..... 23

TANGAZO
Usajili kwa Watafiti na Miradi ya Utafiti ..... 26

Kumbi za Mikutano ..... 28



**Jarida hili huchapishwa mara nne kwa mwaka na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI).**

**Lugha:** Lugha inayotumika katika Jarida hili ni Kiswahili

**Walengwa:** Wadau katika sekta za misitu na ufugaji nyuki

**Malengo:** Jarida hili huchapishwa ili:-

1. Kuhabarisha na kuelimisha umma kupitia tafiti mbalimbali zinazofanywa na kuratibiwa na taasisi.
2. Kutumika kama jukwaa la mawasiliano baina ya watafiti na wadau wa sekta ya misitu na ufugaji nyuki.

**Linatolewa na kusambazwa na:**

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania
S.L.P 1854, Morogoro
Simu: +25523 2935174/2935177
Nakushi: +255 23 2935174
Barua pepe: tafori@tafori.or.tz
Tovuti: www.tafori.or.tz



**Uhariri**
**Mhariri Mkuu**
Dkt. Revocatus Mushumbusi
**Mhariri Mtendaji**
Dkt. Joshua Maguzu

**Wahariri**
Dkt. Siwa Nkya, Dkt. Nancy Pima,
Dkt. Elisha Njoghomi, Bw. Stanslauss Lukiko
**Mhariri Msaidizi**
Bw. Davis Kiwelu, Bi. Lucy Akwilini

**Limesanifiwa na:**
Bw. Davis Kiwelu



# Uoteshaji wa Mianzi  kwa Njia ya Vikonyo Yawa Chachu Katika Kilimo Kibiashara, Uhifadhi wa Mazingira

Utangulizi

Misitu ya Mianzi nchini Tanzania ina eneo linalokadiriwa kuwa na hekta 1,025,033. Misitu hii inapatikana zaidi katika kanda mbili za kiikolojia ambazo ni Nyanda za Juu kusini na Pwani, hivyo kufanya mianzi ya aina tofauti kustawi. Kuna aina kuu nne za mianzi ya asili ambayo kwa majina ya kitaalamu inajulikana kama *Arundinaria alpina (Yushania alpina)*, *Oxytenanthera abyssinica*, *Hickea africana* na *Oreobambos buchwaldii*.

Aidha, mianzi  mingine iliyopo nchini ni ya kigeni, inayojulika kwa majina ya kitaalamu kama *Bambusa bambos, B. multiplex, B. nutans, B. vulgaris, B. balcooa, Dendrocalamus strictus* na *D. nutans*. Mianzi hii ya kigeni imeonyesha uwezo mkubwa wa kustawi katika maeneo mengi hapa nchini, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa haraka na kuwa na ubora unaofanana na baadhi ya miti ya asili ya mbao ngumu. Kwa mfano, mianzi ya asili aina ya *Yushania alpina* imekuwa ikitumika kama nguzo na fito katika maeneo ya Lindi, Songea na Njombe.

Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa za mianzi hapa nchini na kimataifa hususani katika matumizi ya ujenzi, nishati, kutengeneza karatasi, vikapu, samani mbali mbali, pamoja na kuchangia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, mianzi hii inahitaji kustawishwa kwa wingi ili iweze kukabiliana na mahitaji haya.

Kwa kawaida mianzi huchukua muda wa miaka 3 hadi 7 tangu kupandwa mpaka kuvunwa na huchukua takribani miaka 50 mpaka 150 kuishi na baada ya hapo hutoa mbegu na kufa. Kwa sasa, takribani hekta 700 za mianzi zimepandwa kibiashara katika shamba la serikali la miti ya kupandwa Ruvu lililoko Mkoani Pwani kwa kutumia aina mbalimbali.

Pamoja na jitihada zilizofanywa na serikali na jamii za ustawishaji wa mianzi, bado haijastawishwa kwa kiwango kikubwa kutokana na upungufu wa vipando bora. Hii imechangiwa pia na gharama kubwa za mbegu bora. Kwa mfano, kwa soko la nje hususani India na China, mbegu za mianzi huuzwa





Kushoto ni Mianzi jamii ya *Bambusa vulgaris*, na kulia ni jamii ya *Bambusa balcooa*. Picha kutoka Maktaba



Bustani ya mianzi iliyopo TAFORI

takribani shilingi za kitanzania 376,500.00 hadi 627,500.00 kwa kilo moja kutegemeana na aina ya mianzi nje ya gharama za kodi na gharama zingine na hivyo kufanya uwekezaji wa mianzi kuwa wa gharama kubwa. Vilevile, njia mbadala za uoteshaji bado hazijaweza kutumika kwa kiwango kikubwa.

Ili kutatua tatizo hili, TAFORI ilifanya utafiti uliolenga kubaini njia mbadala ya uoteshaji wa mianzi. Hii itasaidia kuongeza uzalishaji wa vipando ili kufidia mahitaji ya kustawishwa kibiashara, kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa jangwa, na uongoaji wa maeneo chini ya Mpango wa Afrika wa Urejeshaji wa Mandhari ya Misitu yaani AFR100.

## Njia mbadala za uoteshaji wa Mianzi

Taasisi ilifanya utafiti wa kubaini njia mbadala ya uoteshaji wa mianzi jamii ya *Bambusa balcooa* na *B. vulgaris.* Spishi hizi zilichaguliwa kutokana na upatikanajii wake katika Shamba la Miti la Ruvu. Sehemu zilizotumika ni vipando vya shina (*culms cuttings*) na matawi (*branch cuttings*) ambavyo vilikusanywa kutoka Shamba la Miti Ruvu na kustawishwa katika bustani ya majaribio iliyopo TAFORI Makao Makuu, Morogoro. Utafiti ulifuatilia uotaji wa vikonyo vya mashina na matawi katika bustani, matumizi ya vichocheo vya kutoa mizizi (*rooting hormone*) na aina ya udongo.

## Matokeo ya utafiti

Utafiti ulibaini kuwa jamii ya mianzi inaweza kuota na kukua vizuri kwa njia ya vikonyo vya mashina (*culms cuttings*) bila kutumia kichocheo cha kutoa mizizi.

## Hitimisho

Mianzi aina ya *Bambusa balcooa* na *Bambusa vulgaris* inaweza kuzalishwa kwa wingi kwa njia mbadala na kwa muda mfupi kwa kutumia vikonyo vya shina (*culms)*. Uoteshaji wa vipando utasaidia kuongeza kasi ya ustawishaji wa mianzi kwa ajili ya kuinua uchumi na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na urejeshaji wa maeneo ya misitu iliyoharibika.

*Makala imeandaliwa na Stephen Maduka, Nancy Pima, Makarius Kavishe, Hanisha Mahiku, Ramadhani Mazige, Raymond Eliud na Alfa Msigala kutoka TAFORI. Kwa mawasiliano zaidi tumia barua pepe tafori@tafori.or.tz*

# Upimaji wa Ubora wa Mbao kwa Tensiomita Kuwa Fursa kwa Wadau wa Misitu



Tensiomita (Tensometer/ Universal Testing Machine) katika maabara ya mbao ya TAFORI

## Utangulizi

Ili kuhakikisha wadau wa sekta ya misitu na ufugaji nyuki wanatumia mbao kwa njia bora, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) imeendelea kuboresha maabara yake ya mbao kwa kuongeza vifaa vya kisasa vinavyotoa majibu yenye uhakika na kwa haraka zaidi. Ili kuendelea kuimarisha maabara hii, Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ulifadhili ununuzi wa mtambo wa kisasa wa kidijitali, ujulikanao kama tensiomita, unaotumika kupima ubora wa mbao kwa kuzingatia sifa muhimu zinazohitajika kwa matumizi mbalimbali.

Tensiomita inapima ubora wa mbao kwa kufuata viwango vya kimataifa (ASTM D143). Upimaji huu husaidia kubaini kama mbao zinakidhi viwango vinavyotakiwa kwa matumizi mbalimbali yakiwemo ujenzi wa nyumba za kawaida, magorofa, madaraja pamoja na utengenezaji wa samani.

## Vipimo vinavyopimwa na Tensiomita

Tensiomita hupima vipimo mbalimbali vya mbao, vikiwemo: kupinda (*static bending test*), mgandamizo (*compression test*), kuvutika (*tension test*), ugumu (*hardness test*), kupasuka (*cleavage test*), na kushika msumari (*nail withdraw test*).



Tensiomita (*Tensometer/Universal Testing Machine*) inayotumika kupima ubora wa mbao katika maabara ya mbao ya TAFORI. Picha na Maktaba

# Vipimo vinavyopimwa na Tensiomita

| Kipimo | Maelezo ya kipimo | Sampuli inayotakiwa (Milimita (mm) | Umuhimu wa kipimo |
|---|---|---|---|
| Upindaji wa mbao (*static bending test*). | Hupima uwezo wa mbao kupinda inapowekewa mzigo katikati, huku ikiwa imeshikiliwa kwenye ncha zake mbili. | 50*50*760 | Kusaidia katika kuchagua mbao zinazofaa kwa matumizi yenye mzigo unaosambazwa au wa kati, Mfano kuezeka, samani, na milango |
| Mgandamizo (*Compression test*) | Hupima uwezo wa mbao kustahimili msukumo unaoelekezwa katika mhimili wake wa urefu *(longitudinal axis*) | 50*50*200 | Kusaidia kuchagua mbao sahihi kwa matumizi ya kiufundi kama vile ujenzi wa nyumba, madaraja, na maghala. |
| Mvutano (*Tension test*) | Hupima uwezo wa mbao kustahimili nguvu ya kuvutwa (*tensile force*) kwenye mhimili wake wa urefu. | 50*50*200 | Kutathmini uimara wa mbao zinazotarajiwa kushikilia au kunyanyua vitu kwa njia ya kuvutwa, kama kwenye kamba, boriti za truss, au fremu za mbao. |
| Ugumu *(Hardness test*) | Hupima uwezo wa mbao kustahimili nguvu ya juu ya msukumo inayopelekea kuchubuka, kubonyea, na kuchakaa. | 50*50*150 | kutathmini uimara wa mbao dhidi ya kuharibika au kubonyea kutokana na nguvu ya juu, hasa kwenye sakafu, mataruma ya reli, au mguu wa samani. |
| Kupasuka (*Cleavage test*) | Hupima uwezo wa mbao kupasuliwa au kugawanyika (cleave) inapowekewa nguvu ya mgawanyiko (*splitting force*), hasa kwenye nyuzi za mbao. | 50*50*200 | Husaidia kujua ukomavu wa mbao na kuchagua mbao zinazofaa kwa kutengeneza vipande vidogo kwa njia ya kupasuliwa kwa ufanisi (kama kuni, nguzo). |
| Kushika msumari (*Nail withdraw test*) | Hupima nguvu inayohitajika kung'oa msumari kutoka kwenye mbao | 76*100*25 | Kuonyesha uwezo wa mbao kushikilia msumari au skurubu, jambo muhimu katika ujenzi wa nyumba, samani, na fremu. |

## Hitimisho

Uwepo wa tensiomita ni fursa kwa wadau mbalimbali katika kutumia mbao ambazo ubora wake unafahamika ili kulinda usalama wa watumiaji. Hivyo, wadau wanaaswa kuendelea kupata huduma ya kupima ubora wa mbao katika maabara ya mbao ya TAFORI.


## Shukrani

Taasisi inatoa shukrani kwa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) kwa kuwezesha kupatikana kwa Tensiomita.



*Makala imeandaliwa na Lugi Kibasi, Makarius Kavishe, Ramadhani Mazige, Hanisha Mahiku, Alfa Msigala, na Pilly Kagosi kutoka Kitengo cha Huduma za Maabara, TAFORI Makao Makuu, Morogoro.*







Kaimu Afisa Mtendaji MKuu wa Mfuko wa Misitu Tanzania TaFF, Dk. Tuli Msuya, ashangazwa na aina ya asali iliyotokana na Utafiti kutoka TAFORI Picha na Maktaba

# Sifa za Asali ya Tanzania Zaonesha Upekee Katika Soko la Kimataifa

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) kupitia kitengo chake cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki imeendelea kufanya tafiti kadhaa katika eneo la ufugaji nyuki. Tafiti zilizofanyika ni pamoja na zile zinazolenga kutatua changamoto za sekta ya ufugaji nyuki katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, utafiti uliokamilika na matokeo kuwafikia wadau ni utafiti wa kubaini sifa za asali ya Tanzania. Matokeo yamekuwa chachu na gumzo chanya kwa wadau wa nyuki na wananchi kwa jumla katika kung'amua masuala muhimu yenye mchango katika kuendeleza na kukuza sekta ya ufugaji nyuki nchini.

Imebainika kuwa asali ya Tanzania kutoka maeneo ya uoto mbalimbali nchini zina sifa tofauti. Sifa zilizozingatiwa katika utafiti huo ni pamoja na ladha, rangi na uwepo wa viambata. Imeonekana kuwa asali kutoka maeneo tofauti zinaambatana na ladha tofauti. Nyingi ni tamu na wakati nyingine zikiwa na uchachu au ukakasi. Sifa nyingine ni rangi, ambapo nyingi ni za kahawia iliyofifia, ikifuatiwa na kahawia yenye mn'gao, kahawia na nyeusi. Asali chache zimebainika kuwa na rangi ya maziwa au nyeupe.

Aidha, sifa nyingine ni uwepo wa viambata; ambapo asali nyingi zimeonesha kuwa na viambata vyenye nguvu ya kuua bakteria na kuvu. Aidha, baadhi ya asali zimepatikana kuwa na kampaundi aina ya *Chrysin* na *quercetin* ambazo zina uwezo wa kuzuia ueneaji wa seli za saratani. Kwa muktadha huo, asali inaweza kutumika katika tiba za magonjwa mbalimbali ya binadamu na wanyama wa kufugwa pale ambapo utafiti wa kubaini kiwango utakapofanyika.

Matokeo ya sifa za asali yamewezesha kuandaliwa kwa chapa ya asali ya Tanzania ambapo Taasisi imeshirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na wadau wengine. Chapa hii ilizinduliwa na Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii katika hafla iliyofanyika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora tarehe 4 Oktoba, 2024.









Uzinduzi wa Chapa ya Asali ya Tanzania. Picha kutoka Maktaba




Wadau washangazwa na rangi ya asali iliyotokana na Utafiti katika Maonesho ya Sabasaba 2025 . Picha na Maktaba



Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Chana (Mb) (katikati) katika uzinduzi wa nembo ya asali ya Tanzania itakayotumika kuitambulisha bidhaa hiyo katika soko la dunia. Picha na Maktaba

Aidha, matokeo ya sifa za asali yemesambazwa kupitia majukwaa mbalimbali yakiwemo Kongamano la Tatu la Kisayansi la TAFORI llilofanyika Desemba, 2024, Siku ya Misitu Duniani iliyoadhimishwa Kitaifa Mkoani Njombe mwezi Machi, 2025, Siku ya Nyuki Duniani iliyoadhimishwa Kitaifa Mkoani Dodoma mwezi Mei, 2025 na Maonesho ya Sabasaba na Nanenane ya mwaka 2025.

Matokeo ya utafiti na chapa ya asali iliyozinduliwa ni fursa kwa wadau kutafuta masoko kulingana na sifa na chanzo cha asali.

## Shukrani

Taasisi inatoa shukrani kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mfuko wa Misitu Tanzania, Mradi wa Kuboresha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (BEVAC), na Kituo cha Biashara cha Kimataifa (ITC) kwa uwezeshaji.

*Makala imeandaliwa na Allen Richard, Stanslauss Lukiko, Pilly Kagosi na Stephen Msemo, Kitengo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki, TAFORI Makao Makuu Morogoro*



Moja ya aina ya asali iliyotokana na Utafiti kutoka TAFORI. Picha na Maktaba



# Ufugaji wa Nyuki Wasiodunga, Rafiki kwa Maeneo ya Makazi

## Utangulizi

Nyuki wasiodunga wanafahamika pia kama nyuki wasiouma au nyuki wadogo. Hata hivyo sio sahihi sana kuwaita nyuki wadogo, maana katika baadhi ya nchi nyuki wa aina hii wameonekana kuwa wakubwa kuliko nyuki wanaodunga. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) imefanya utafiti wa kubaini aina ya nyuki wasiodunga wanaofaa kufugwa, namna endelevu ya kupata makundi yake na mbinu za kuwafuga katika maeneo ya makazi.

Utaratibu rafiki kwa rika zote na jinsia kushiriki kufuga nyuki jirani na makazi utaandaliwa kwa kuzingatia majawabu ya kitafiti kutoka katika maeneo yaliyobainishwa kuwa na makundi yanayoweza kuhamishwa na kufugwa sehemu mbalimbali nchini.

Taasisi inaratibu utekelezaji wa utafiti huu unaoshirikisha timu ya utafiti ambapo watafiti watatu ni kutoka TAFORI, wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), mmoja mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) – Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), TFS na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) Tabora.



*"Tafiti zimebaini kuwa mzinga mmoja huzalisha wastani wa kilo 2 – 4. Aidha, imebainika kuwa bei ya asali hii ni wastani wa shilingi 25,000 kwa kilo ya asali"*. Picha na Maktaba








Aina za mizinga na ufugaji wa nyuki wasiodunga katika maeneo mbalimbali nchini. Picha kutoka Maktaba

## Uchambuzi na ziara za uwandani

Matokeo ya awali yaliyopatikana katika machapisho mbalimbali na ziara za uwandani yamebainisha kuwa kuna spishi 12 za nyuki wasiodunga ambazo zinapatikana katika maeneo mbalimbali nchini.

Uchambuzi umeonesha kuwa spishi zinazopoatikana kwenye jenasi ya *Meliponula* na *Hypotrigona* ndizo zinazofaa kwa uzalishaji wa asali. Makundi ya nyuki wasiodunga katika jenasi hizi mbili hayapatikani kwa wingi na hii imepelekea wanajamii kuwinda makundi kwenye misitu kadhaa na kwenda kufugia majumbani au kuwauzia wanaohitaji kufuga.

Aidha utafiti umebaini kuwa; wanajamii wengi nchini wamekuwa na mwamko wa kutafuta makundi ya nyuki. Kutokana na uhaba, bei ya kundi huanzia shilingi za kitanzania 25,000 hadi 250,000.

Tafiti zimebaini kuwa mzinga mmoja huzalisha wastani wa kilo 2 – 4. Aidha, imebainika kuwa bei ya asali hii ni wastani wa shilingi 25,000 kwa kilo ya asali. Utafiti huu ulifanyika katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Geita, Kagera, Mbeya, Katavi, Rukwa, Pwani, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Kaskazini Unguja, Mjini,Magharibi, Kusini Pemba na Kaskazini Pemba pamoja na Morogoro.

## Hitimisho

Utafiti wa ufugaji wa nyuki wasiodunga unaendelea katika maeneo tisa (9) yaliyobainishwa kuwekwa mizinga iliyoboreshwa yenye makundi katika mabanda ya nyuki yaliyobuniwa kwa ajili ya majaribio katika mikoa ya Mbeya, Katavi, Kagera, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Pwani, Tanga na Mjini Magharibi.

*Makala imeandaliwa na Kitengo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki, TAFORI Makao Makuu Morogoro.*



Muonekano wa Kituo cha TAFORI cha Utafiti Kibaha baada ya kukamilika kwa ukarabati, kupitia ruzuku ya TaFF. Picha na Maktaba

# TAFORI Yaboresha Mazingira ya Utendaji Kazi Kupitia Ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)

## Utangulizi

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) hutekeleza majukumu yake kupitia vituo vya utafiti ambavyo ni Kibaha, Lushoto, Moshi, Dodoma, Mafinga, Malya, na Tabora. Vituo vya Utafiti wa Misitu Kibaha na Malya vina jukumu la kufanya tafiti za miti ya asili na ya kigeni inayofaa kupandwa na kukua katika maeneo ya ukanda wa Pwani na ukanda wa Ziwa. Majengo ya ofisi ya vituo hivi yalijengwa kati ya mwaka 1973-1979.

Kutokana na uchakavu wa majengo ya ofisi katika vituo hivi, Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ulitoa ruzuku kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi za Kibaha, Malya na Tabora.

Ruzuku hiyo imewezesha kuweka mazingira bora zaidi ya kazi yenye ufanisi na tija. Maboresho haya yameimarisha uwezo wa vituo katika kufanya tafiti muhimu, na hivyo kuchangia katika tafiti mbalimbali zinazosaidia katika upandaji miti, uanzishwaji wa mashamba ya miti na utunzaji wa misitu katika maeneo ya Pwani na Kanda ya Ziwa, Tanzania. Maboresho yaliyofanyika ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi, mafunzo na ukarabati wa majengo.

## Ununuzi wa vitendea kazi

Katika hatua ya kuimarisha uwezo wa taasisi ili iweze kutoa huduma bora na kuboresha usimamizi wa





*Muonekano wa jengo la Kituo cha Utafiti Kibaha kabla ya ukarabati kupitia ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF).* Picha na Maktaba

rasilimali za misitu na nyuki, taasisi kupitia ufadhili wa TaFF imefanya manunuzi ya kompyuta za mezani na mpakato pamoja na magari mawili (*4WD pickup double cabin*).

## Mafunzo

Aidha, katika hatua nyingine ya kujenga uwezo kwa watumishi, TaFF iligharamia mafunzo ya kujenga uwezo wa kuandika maandiko bora ya utafiti kwa lengo la kushawishi upatikanaji wa fedha za utafiti. Mafunzo haya yaliongozwa na Taasisi kwa kushirikiana na Mtaalam wa utafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Misitu Kenya (KEFRI). Mafunzo haya yalisaidia pia katika kubadilishana uzoefu na ujuzi kati ya TAFORI na KEFRI.

## Ukarabati wa majengo

Taasisi kupitia TaFF imefanya ukarabati wa majengo ya ofisi za vituo vya Utafiti wa Misitu: Kibaha (Mkoani Pwani), Kituo cha Utafiti wa Misitu Malya (Mkoani Mwanza) na ujenzi wa ofisi ya Kituo cha utafiti wa Miti ya Miombo Tabora (Mkoani Tabora).

## Hitimisho

Ukarabati wa majengo ya ofisi za vituo vya TAFORI Kibaha na Malya umeboresha kwa kiasi kikubwa mazingira ya kazi kwa watumishi. Ukarabati huu umehamasisha wafanyakazi kuongeza ari na dhamira ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa ufanisi zaidi.

*Makala imeandaliwa na Nancy Pima, Msumi Mkomwa, Idd Dibwa na Rehema Ngalile. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Kituo cha Utafiti wa Misitu Kibaha, S.L.P 30021, Kibaha, Pwani na Kituo cha utafiti wa Misitu Malya, S.L.P 166, Malya.*



Muonekano wa jengo kabla (kushoto) na baada ya kukamilika kwa ukarabati katika Kituo cha Utafiti Malya. Picha kutoka Maktaba





# Tafiti za Udongo Zabainisha Njia Sahihi za Upandaji Miti Kwenye Maeneo Sahihi

## Utangulizi

Utafiti wa udongo ni hatua muhimu katika kuhakikisha upandaji wa miti unaleta matokeo bora na endelevu. TAFORI kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imewezesha kufanya tafiti zilizosaidia kuandaa miongozo ya kitaalamu kuhusu aina sahihi za miti ya kupandwa kulingana na ubora wa udongo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, chambuzi mbalimbali zilizofanywa na TAFORI ni zile zinazolenga uanzishaji wa mashamba ya miti na utunzaji wa vyanzo vya maji, ikiwemo Shamba la Miti Morogoro, Shamba la Miti Silayo -Geita, Shamba la Miti Nzega -Tabora, Shamba la Miti Mwese - Katavi, Shamba la Miti Rwamugasa - Geita, Shamba la Miti Makere -Kigoma, Shamba la Miti Buhigwe-Kigoma, Shamba la Miti Mpepo-Ruvuma, pamoja na Chanzo cha Maji Mzakwe-Dodoma.

Udongo una sifa tofauti za rutuba, kina, tindikali au besi, na uwezo wa kushikilia maji. Sifa hizi zina mchango au kuathiri moja kwa moja ukuaji wa miti. Utafiti wa udongo husaidia kutambua maeneo yanayofaa kwa upandaji wa spishi za miti, kulingana na udongo husika hivyo kuongeza uwezekano wa miti kustawi na kutoa mazao bora.

## Hatua muhimu tatu za kufuata kwenye utafiti wa udongo:

i) Ukusanyaji wa Sampuli za Udongo

Sampuli za udongo zinapaswa kuchukuliwa kutoka kwenye pointi nne zinazofunika eneo la mraba wa mita 20 kwa 20. Sampuli za udongo zisizo na msuguano zinakusanywa kutoka tabaka mbili tofauti za udongo; udongo wa juu kutoka sentimita (sm) 0 hadi 20 na udongo wa chini kutoka sm 20 hadi 40.

Tabaka hizi zinaonesha kina ambacho kuna upatikanaji mkubwa wa virutubisho vya udongo. Sampuli zinazokusanywa hufungwa mara moja na kuwekwa alama zikiwa shambani. Sampuli kutoka kila mraba zinapaswa kuchanganywa ili kuunda sampuli ya udongo iliyochanganywa ambayo itatumika kwa uchambuzi katika maabara.

ii) Maandalizi ya Sampuli za Udongo katika Maabara

Sampuli za udongo hukaushwa, husagwa na kuchujwa kabla ya kuchambuliwa. Mchakato wa kusaga na kuchuja hufanyika ili kuhakikisha mchanganyiko wa udongo unawiana kwa ajili ya uchambuzi. Udongo uliokauka husagwa kwa kutumia kisaga cha mitambo na hupitishwa kwenye chujio cha waya wenye ukubwa wa takriban milimita mbili.

iii) Uchambuzi wa sampuli za udongo kuangalia sifa za umbo na kemikali

Uchambuzi wa udongo ili kuangalia sifa za umbo na kemikali unafanyika katika maabara ya TAFORI na baadhi ya vipimo kwa kushirikiana na Maabara zilizopo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Milingano, na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Morogoro, na Chuo cha Ufundi Arusha.

## Baadhi ya matokeo ya utafiti wa udongo nchini kwa ufupi

a) Baadhi ya miti, hususani jamii ya misindano na mikaratusi hustawi vizuri kwenye maeneo yenye udongo wa tindikali ya juu (pH ya wastani wa 4.5) na unaoweza kushikilia unyevu.

b) Mchanganyiko wa udongo wa msituni, mchanga na samadi hutoa matokeo bora katika ukuzaji wa miche ya miti.

c) Aina ya miti inayopendekezwa kwa maeneo yenye udongo wenye tindikali ni tofauti na zile zenye udongo wenye besi, hivyo uchaguzi sahihi wa aina ya miti ni muhimu.



*"Sampuli zinazokusanywa hufungwa mara moja na kuwekwa alama zikiwa shambani, pia Sampuli hizi za udongo hukaushwa, husagwa na kuchujwa kabla ya kuchambuliwa"*

**Sifa za udongo na aina ya miti inayofaa kupandwa kwenye baadhi ya Mashamba ya Miti nchini.**

| NA: | KANDA | SHAMBA | MKOA | WASTANI WA TINDIKALI/NYONGO | AINA YA MITI INAYOPENDEKEZWA KUPANDWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ziwa | Silayo | Geita | 3.9-5.0 | Msindano, Mkaratusi, Mgrivelia na Muhumula |
| 2 | Mashariki | Morogoro | Morogoro | 5.6-6.5 | Mkaratusi na Mgunga |
| 3 | Magharibi | Mwese | Katavi | 4.4-6.0 | Msindano, Mkaratusi, Mgrivelia na Mgunga |
| | | Mwanhara | Tabora | 4.6-6.2 | Mkaratusi, Mgunga na Mvinge |
| | | Makele | Kigoma | 5.5-7.7 | Mtiki, Muhumula, Mkaratusi, Msidano na Mvule |
| 4 | Kaskazini | Shume | Tanga | 3.83-6.09 | Msindano, Mkaratusi na Cypress |
| 5 | Nyanda za Juu kusini | Sao Hill | Iringa | 4.0-5.05 | Msindano na Mkaratusi |
| | | Mpepo | Ruvuma | 4.8-6.3 | Msindano, Mitiki, Mkaratusi na Mtiki mweupe |
| 6 | Kusini | Machang'anja | Lindi | 6.6-6.8 | Mtiki, Mkaratusi na tiki nyeupe |
| | | Ziwani | Mtwara | 4.93 - 6.89 | Msindano, Mgunga, Mkaratusi na Mtiki |

## Hitimisho

Kwa ujumla, utafiti wa udongo unaofanywa na TAFORI umechangia kwa kiasi kikubwa kutoa majawabu ambayo ni mazuri katika kuendeleza mashamba ya miti kwa upandaji wa aina sahihi ya miti.

Aidha, uchaguzi sahihi wa aina ya miti kulingana na sifa za udongo, umeongeza tija, uhifadhi wa mazingira na upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu nchini Tanzania.

*Makala imeandaliwa na Joshua Maguzu na Amani Uisso kutoka TAFORI Makao Makuu, na Nancy Pima kutoka TAFORI Kituo cha Kibaha. Kwa mawasiliano zaidi tumia barua pepe: tafori@tafori.or.tz*



**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**
**TANZANIA FORESTRY RESEARCH INSTITUTE**

# APPLICATION FORM FOR REGISTRATION OF FORESTRY RESEARCHER

(Submit soft and hard copy)

**PART A**

1. Surname.........................................................................................................
Other names...............................................................................
Physical address ...................................................................................
Email Address............................................... Phone Number............................
2. Citizenship:....................................... Country of origin:.......................................
Institutional affiliation:.........................................................................................
Mailing address (outside Tanzania):...........................................................................
3. Academic qualifications (Start with most current);

Attach current passport size photo

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

4. Referees' names and addresses (two referees preferably one of whom must be based in Tanzania)
(a) .....................................................................................................
..........................................................................................................................................
(b) .....................................................................................................
..........................................................................................................................................
5. Recent publications:
(a) ..................................................................................................
(b) ..................................................................................................
(c) ..................................................................................................
(d) ..................................................................................................
6. Society Membership (if any):
(a) .................................................................................................
(b) .................................................................................................
(c) .................................................................................................
7. Attach current curriculum vitae (CV) and certifies copies of academic certificates

Signature of the applicant ......................................................................... Date: ...........................

PART B

FOR OFFICE USE
Research registration number ...........................................................................
Recommendation...........................................................................................
.......................................................................................................
.......................................................................................................
Signature ................................................ Date: ............................

Official stamp Official stamp

***To be able to register online please visit out website: www.tafori.or.tz***



# TAFORI Yafanikisha Kongamano la Tatu la Kimataifa la Kisayansi

## Utangulizi

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) ilifanikiwa kuandaa Kongamano la tatu la Kimataifa la Kisayansi lenye kaulimbiu: "Kurejesha Mandhari ya Misitu kwa Maendeleo Endelevu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia ya nchi." Kongamano hilo la siku tatu lilifanyika kuanzia tarehe 11 hadi 13 Desemba 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), Arusha, Tanzania.

Lengo kuu la kongamano hili lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano kati ya wadau wa misitu na ufugaji nyuki kwa kutoa jukwaa la kubadilishana maarifa ya kisayansi, ubunifu, uzoefu na mikakati ya kuchochea mijadala yenye tija na kuibua mikakati ya utekelezaji katika kusaidia juhudi za urejeshaji wa mandhari ya misitu na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

## Washiriki wa Kongamano

Kongamano hili lilikutanisha washiriki zaidi ya 900 kutoka nchi mbalimbali. Washiriki walijumuisha watafiti, watunga sera, wajasiriamali, wataalamu wa sekta mbalimbali, wadau, pamoja na wanafunzi kutoka Tanzania na nje ya nchi. Wajumbe walitoka katika nchi kama vile Kenya, Ujerumani, Uswisi, Estonia, Uholanzi, Japani, Zambia, na Afrika Kusini, hali iliyochangia kuunda mazingira tajiri ya kubadilishana maarifa ya kisayansi, ubunifu, na uzoefu.

Ushiriki huu uliimarisha majadiliano na kuimarisha juhudi za pamoja za kurejesha mandhari ya misitu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## Ufunguzi wa Kongamano

Ufunguzi wa kongamano uliongozwa na Mheshimiwa Bw. Dunstan Kitandula (MB) Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambaye alifungua rasmi kongamano kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi wengine walioambatana na Mgeni Rasmi ni pamoja na Prof. Veridiana Masanja, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TAFORI, Dkt. Revocatus Mushumbusi, Mkurugenzi Mkuu wa TAFORI, na Bw. Jackson Msome, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki (NABAC). Sherehe za ufunguzi zilipambwa na Bendi ya Polisi Tanzania na zilianza na uzinduzi rasmi wa Maonyesho ya Kongamano





Mgeni Rasmi, Mhe. Bw. Dunstan Kitandula (MB) Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii akitoa hotuba rasmi ya ufunguzi. Picha na Maktaba



Mkurugenzi Mkuu wa TAFORI Dkt. Revocatus Mushumbusi wakati wa sherehe za ufunguzi. Picha na Maktaba



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TAFORI Prof. Verdiana Masanja wakati wa sherehe za ufunguzi. Picha na Maktaba

la Kimataifa la Kisayansi na Mgeni Rasmi Bw. Dunstan Kitandula (MB)

## Hotuba ya Mgeni Rasmi

Mheshimiwa Bw. Dunstan Kitandula (MB), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, alitoa hotuba rasmi ya ufunguzi kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Makamu wa Rais alitoa shukrani zake kwa programu za sekta ya misitu na ufugaji nyuki. Muhtasari wa hotuba ya Mgeni Rasmi ulijumuisha:

- Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), kupitia taasisi zake na Mfuko wa Misitu Tanzania, inapaswa kutenga fedha kusaidia tafiti zinazoshughulikia changamoto katika sekta za misitu, ufugaji nyuki, na mazingira.
- TAFORI, kwa kushirikiana na taasisi nyingine za utafiti, inapaswa kufanya tafiti ili kutafuta suluhisho la kudhibiti aina za mimea vamizi ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.
- TFS inapaswa kuandaa mipango mahususi ya kukabiliana na kuzuia moto wa misitu katika misitu ya asili na mashamba ya miti.
- Kuandaa kampeni za kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa misitu, ufugaji nyuki, na jinsi ya kushiriki katika shughuli za urejeshaji.







Mwasilishaji wa bango akiwasiliana na washiriki kwenye kongamano. Picha na Maktaba

- Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi, na serikali za mitaa ili kuunda mikakati ya pamoja ya urejeshaji misitu.
- Kutoa mafunzo kwa wakulima na jamii kuhusu mbinu endelevu za kilimo, ufugaji nyuki, na uhifadhi wa misitu, na kuandaa na kutekeleza sera zinazounga mkono urejeshaji misitu na usimamizi endelevu wa rasilimali.
- Kuimarisha miundombinu katika maeneo ya mashamba ya miti na kuwezesha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za misitu na ufugaji nyuki ili kukuza uzalishaji wa bidhaa zenye ubora wa juu.
- Wizara husika zinazohusika na uratibu wa biashara ya kaboni zinapaswa kutenga fedha kwa taasisi za utafiti, ikiwemo TAFORI, kufanya tafiti zinazolenga kuongeza faida za nchi kutokana na biashara ya kaboni.

## Uwasilishaji wa Kitaalamu

Kaulimbiu kuu iligawanyika katika mada ndogo nane (8), Jumla ya machapisho 81 yaliwasilishwa, mawasilisho ya bango 12, na mawasilisho ya mdomo 60. Mada ndogo zilizofanyiwa mawasilisho ni kama ifuatavyo;

1. Uwasilishaji kuhusu Ufadhili wa Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki

Utafiti uliwasilishwa ukichambua masuala mbalimbali ya ufadhili wa miradi ya upandaji miti na ufugaji nyuki kwa ajili ya kuharakisha urejeshwaji wa mandhari na mfumo ikolojia.

2. Uwasilishaji kuhusu Uharibifu wa Misitu, Uhifadhi wa Bioanuwai na Suluhisho la Kiasili

Ilizungumzia tishio la kuenea kwa miti vamizi isiyo ya asili katika mifumo ya ikolojia ya Afrika Mashariki. Utafiti ulihusu mifumo mbalimbali ya ikolojia kama vile uhifadhi wa mikoko nchini Kenya na mifumo ya kilimo-msitu nchini Tanzania.

3. Uwasilishaji kuhusu Ubunifu na Teknolojia katika Sekta ya Misitu na Nyuki

Ilijikita katika matumizi ya machine learning kwenye urejeshaji wa misitu na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Utafiti ulichunguza mifumo ya moto katika misitu ya Tongwe West, uvamizi wa nyuki na nzi wa tachinid, na mbinu za kuhifadhi mbao. Pia ulijadili matumizi ya teknolojia ya kijiografia katika uvunaji wa miti, sifa za asali zenye viambata vya kupambana na bakteria, na uvumbuzi wa aina mpya ya Sansevieria.

4. Uwasilishaji kuhusu Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Misitu na Nyuki katika Mabadiliko ya Tabianchi

Ilihusu mienendo ya mnyororo wa thamani wa bidhaa za misitu na nyuki katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi. Utafiti ulijadili mifumo ya msaada kwa wafugaji nyuki, usambazaji wa mizinga na athari zake kwa uzalishaji wa asali.

5. Uwasilishaji kuhusu Mtazamo wa Kijinsia katika Sekta ya Misitu na Nyuki

Ilitoa muhtasari wa hali ya usawa wa kijinsia katika sekta ya misitu na nyuki. Machapisho ya utafiti katika mada hii yalijadili masuala kama vile mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki katika Kaunti

ya Kitui, Kenya, na ushiriki wa wanawake katika maeneo ya mnyororo wa thamani wa mbao ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

6. Uwasilishaji kuhusu Sera na Utawala wa Uchumi wa Kijani na Buluu

ilijadili mchango wa sera za misitu katika kufanikisha malengo ya kitaifa ya uchumi wa kijani na buluu, kwa kutumia uzoefu wa Tanzania. Utafiti ulijikita katika kuboresha ufanisi katika mnyororo wa thamani wa mbao zilizokatwa kama mkakati wa kusaidia uchumi, kupunguza ukataji miti hovyo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

7. Uwasilishaji kuhusu Suluhisho la Nishati Safi kwa Uendelevu wa Mandhari ya Misitu

ilieleza masuluhisho ya nishati safi kwa ajili ya kudumisha mifumo ya misitu nchini Tanzania. Utafiti ulihusisha uchunguzi kuhusu uhalalishaji wa biashara ya mkaa, athari za matumizi ya kuni na mkaa kwa mazingira, na uchambuzi wa sera na sheria zinazokwamisha uendelevu wa mnyororo wa thamani wa mkaa.

8. Uwasilishaji kuhusu Utawala na Usimamizi wa Urejeshaji wa Mandhari ya Misitu

Ilijadili nafasi ya wazalishaji wa misitu na mashamba katika utekelezaji wa urejeshaji na athari za utawala kwenye utekelezaji wa FLR. Utafiti ulichunguza changamoto za usambazaji wa matokeo ya tafiti, tathmini ya ukuaji wa kloni za mikaratusi kwa miaka 6, na utawala wa misitu kupitia uchambuzi wa machapisho ya kisayansi.

## Mawasilisho ya Mabango

Mabango yalionyeshwa katika ukumbi wa mapokezi kwenye chumba cha kongamano kwa muda wa siku tatu, na watoa mada walikuwepo kuingiliana na washiriki.

## Maonesho

Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha, kilitoa nafasi nzuri na rahisi kufikiwa kwa ajili ya maonesho. Kulikuwa na waonyeshaji 21 kutoka taasisi za umma na sekta binafsi. Wote walionesha bidhaa mbalimbali za misitu na ufugaji nyuki, jambo lililoonyesha mchango wa sekta hiyo. Zaidi ya hayo, mgeni rasmi pia alipata fursa ya kutembelea vibanda vyote vya maonesho kwenye kongamano.



Mgeni Rasmi, Mhe. Felician Mtahengerwa akitoa hotuba kwenye sherehe ya kufunga kongama. Picha na Maktaba

## Sherehe ya Kufunga

Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Bw. Felician Mtahengerwa (Mkuu wa Wilaya ya Arusha), ambaye alimwakilisha Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (MB), Waziri wa Maliasili na Utalii. Bw. Mtahengerwa alifunga rasmi Kongamano la 3 la Kimataifa la Kisayansi la TAFORI, akitambua michango muhimu ya tukio hilo katika kukabiliana na changamoto katika sekta za misitu na ufugaji nyuki. Bw. Mtahengerwa alisisitiza umuhimu wa kurejesha mandhari ya misitu kwa ajili ya maendeleo endelevu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kama ilivyolingana na mada ya kongamano hili. Muhtasari wa hotuba ya Mgeni Rasmi ulijumuisha:

- Taasisi za utafiti ziendelee kufanya tafiti zinazoshughulikia changamoto zinazoikabili sekta za misitu na ufugaji nyuki.
- Washirika wa maendeleo waendelee kushirikiana na serikali na taasisi zake za utafiti ili kupata fedha kwa ajili ya mipango mbalimbali ya utafiti nchini.
- Wataalam na wananchi wawe tayari kukubali na kutumia matokeo ya utafiti yanayotolewa na watafiti wetu.

Mgeni Rasmi aliwashukuru washiriki wote, wawasilishaji, na waonyeshaji kwa ushiriki wao hai na michango yao katika masuala mbalimbali yanayohusu bidhaa za misitu na ufugaji nyuki. Mgeni Rasmi alitoa wito kwa wadau kuendeleza juhudi za kuhakikisha maendeleo endelevu ya sekta za misitu na ufugaji nyuki.



Mgeni rasmi na washiriki wengine wakimsikiliza mtafiti kutoka TAFORI kwenye uwanja wa maonyesho wa kongamano. Picha na Maktaba




Wataalam wa TAFORI na Urusi wakiwa katika picha ya pamoja, TAFORI Makao Makuu, Morogoro, Tanzania. Picha na Maktaba



Mtaalamu kutoka TAFORI Dkt. Chelestino Balama akiwasilisha mafanikio ya utafiti yaliyofikiwa, na Bi. Mariia Kuzko kutoka Chuo Kikuu cha Saint Petersburg State Forest, Urusi akifuatilia kwa karibu. Picha na Maktaba



# TAFORI Yaanzisha Mashirikiano na Chuo Kikuu cha Saint Petersburg State cha Urusi Katika Kuimarisha Utafiti wa Misitu na Nyuki Nchini

## Utangulizi

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) imepewa jukumu la kufanya, kusimamia tafiti za misitu na nyuki hapa nchini. Utafiti huu hufanyika kwa kufuata vipaumbele vya nchi. Katika kutimiza jukumu hili la utafiti, TAFORI imekuwa ikishirikiana na Taasisi za ndani ya nchi na zile za nje ya nchi. Hivi karibuni TAFORI imefanikiwa kupata mashirikiano ya Kimataifa na Chuo Kikuu cha Saint Petersburg State, cha Urusi. Katika jitihada za kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika utafiti wa misitu na nyuki, ujumbe wa wanasayansi kutoka nchini Urusi walitembelea TAFORI, mwezi Machi, 2025 na kufanya mkutano kwa ajili ya kujadili maeneo ya mashirikiano.

Wataalamu wa TAFORI na Urusi walikaa pamoja na kujadili masuala mbalimbali yakiwepo maeneo ya utafiti ambayo yanaweza kufanywa kwa ushirikiano hasa katika kuimarisha uhusiano wa kisayansi, kielimu na kiteknolojia kati ya Tanzania na Urusi.

Katika mkutano huo, TAFORI iliwasilisha mafanikio yaliyopatikana kutokana na tafiti zake za msingi ikiwa ni pamoja na 1) tafiti za kuhifadhi na kuboresha spishi za miti asilia zilizo hatarini kutoweka nchini; 2) upembuzi yakinifu na kutathmini uwezekano wa kuanzisha mashamba mapya ya misitu nchini; 3) afya ya misitu; 4) mbinu zinazotumika kudhibiti mimea vamizi; 5) mtawanyiko wa rasilimali misitu na viwanda; 6) ubora wa mbao ili kuboresha matumizi yake katika tasnia ya misitu; 7) utatuzi wa changamoto zinazokabili sekta ya ufugaji nyuki nchini; na 8) ubora wa asali inayozalishwa Tanzania. Katika wasilisho hili, TAFORI ilibainisha fursa za kushirikiana katika nyanja za ikolojia, matumizi endelevu ya mazao ya misitu, usimamizi wa misitu, na teknolojia za uhifadhi wa mazingira kwa ujumla. Pamoja na eneo hili la utafiti, masuala ya kujenga uwezo wa watafiti na mazingira yake pia yatahusika. Eneo lingine ambalo litajengewa uwezo ni uanzishwaji wa kituo cha umahili wa sayansi ya misitu na elimu.

Katika Mkutano huo, Viongozi akwepo Mkurugenzi Mkuu wa TAFORI Dkt. Revocatus Mushumbusi na Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo (ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TAFORI), walisisitiza umuhimu wa ushirikiano huu katika kuimarisha tafiti ambazo zitalenga kutatua changamoto zinazoikumba sekta ya misitu na nyuki, kama vile mabadiliko ya tabianchi, magonjwa ya mimea na nyuki, na matumizi ya teknolojia za kisasa, ikiwemo matumizi ya satelaiti na ndege nyuki katika usimamizi wa misitu na nyuki.

Mashirikiano yaliyoanzishwa kati ya TAFORI kupitia Chuo kikuu cha Saint Petersburg State Forest ni fursa kubwa katika kuimarisha utafiti wa misitu na nyuki. Kupitia ushirikiano huu, watafiti watajengewa uwezo katika maeneo tofauti ya umahili. Kupitia mashirikiano haya, kutakuwepo na shughuli zinazohusiana na utalii ikolojia utakaofanywa na wataalamu wetu wa ndani na kutoka Urusi, na hivyo kuongeza pato la Serikali.

*Makala imeandaliwa na Chelestino Balama.*

# TAFORI, WWF, MCDI Zaimarisha Umoja wa Vijiji Vyenye Hifadhi ya Misitu  Kusini mwa Tanzania





Wajumbe wa Mkutano wa kuanzisha UVIHIMI – Mtama.

## Utangulizi

Kuna methali maarufu ya Kiafrika isemayo, 'Ukitaka kwenda haraka, nenda peke yako; ukitaka kufika mbali, nenda pamoja na wenzako.' Methali hii naihusianisha na umuhimu wa ushirikiano na mshikamano kama nguzo muhimu za kufanikisha malengo ya muda mrefu, ikiwemo malengo ya pamoja ya kuhifadhi misitu, kulinda bioanuwai, na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano haswa katika usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu, kumekua na juhudi za kuunganisha vijiji vilivyoko katika hifadhi ya Misitu kupitia uanzishwaji wa Umoja. Juhudi hizi zimefanywa na TAFORI, Shirika la Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira Duniani (WWF), Shirika la Maendeleo ya Mpingo (MCDI), kwa kushirikiana na Halmshauri za Wilaya pamoja na vijiji vilivyoko katika Hifadhi za Misitu.

Ushirikiano huu unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu ya 1998, inayohimiza ushiriki wa jamii katika usimamizi wa Misitu kupitia Usimamizi wa Misitu ya Jamii, katika kuboresha hali ya misitu, utawala bora, na maisha ya jamii zilizo katika Hifadhi za Misitu. Usimamizi wa Misitu ya Jamii hutekelezwa katika ardhi ya vijiji, hususani katika misitu inayomilikiwa au kusimamiwa na Halmashauri ya Kijiji ambapo vijiji vinamamlaka ya kuanzisha na kusimamia Msitu wa Hifadhi wa Kijiji utakosimamiwa na Kamati ya Maliasili na Kijiji.

## Sababu za kuanzisha Umoja na hasara za kutokuwa na umoja

Sababu kuu ya kuanzishwa Umoja wa Vijiji vyenye Hifadhi ya Misitu (UVIHIMI) nikutoa fursa kwa wanajamii kuwa na  Jukwaa la pamoja la kuwezesha vijiji vilivyoko katika Hifadhi za Misitu kuwa na ushirikiano wa pamoja katika kuwasiliana na kubadilishana uzoefu na Mawazo kama ilivyo kwa Muungano wa Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania unaofahamika, kama Community Wildlife Management Areas Consortium (CWMAC), Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), Umoja wa Vyama vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU) na vinginevyo.

Hivyo, Umoja wa Vijiji vinavyotekeleza Usimamizi wa Misitu ya Jamii yaani UMJ utakuwa chombo muhimu katika ngazi ya Wilaya na Taifa kwa; Moja, kuwa jukwaa la mawasiliano, ushirikiano, na kubadilishana uzoefu na mawazo kuhusu UMJ, Mbili, kuwa taasisi huru na

ya kujitegemea kwa ajili ya kufanya ushawishi na kutetea sera na sheria zinazolinda na kuendeleza maslahi ya vijiji, na Tatu, kujenga nguvu ya pamoja ya kushughulikia changamoto zinazovikabili vijiji vinavyotekeleza umoja huo.

Ifahamike kuwa kukosekana kwa Umoja kunasababisha vijiji kufanya kazi za uhifadhi kwa kujitenga, na hivyo kusababisha ugumu katika kutatua changamoto za pamoja kama vile ukosefu wa masoko ya mazao ya misitu, na uvamimizi wa hifadhi za misitu. Aidha, kukosekana kwa umoja huo hupelekea wanakijiji kushindwa kuwasilisha changamoto zinazowahusu katika ngazi mbalimbali za kimaamuzi na kukosa wawakilishi watako shiriki katika majukwaa ya juu ya maamuzi au mabaraza ya ushauri ili kuwakilisha na kutetea maslaihi ya pamoja.

## Juhudi za TAFORI, MCD, WWF kwenye mchakato wa kuimarisha UVIHIMI

Mnamo mwaka 2020, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Finland kupitia mradi wa FORVAC yaani *Forestry and Value Chains Development Programme*, ilianzisha mchakato wa kuandaa mazingira ya kuanzishwa kwa Umoja wa kitaifa. Mchakato huu uliosimamiwa na TAFORI ulihusisha mikutano ya wadau, warsha na tafiti zilizolenga kubaini aina bora ya muundo wa Umoja.



Baadhi ya wajumbe wa Mkutano wa UVIHIMI uliofanyika PTA, Mtwara. Picha na Maktaba



Wajumbe wa Mkutano wa kuanzisha UVIHIMI – Rufiji. Picha na Maktaba

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TAFORI, inasema Umoja huo utaundwa katika ngazi ya wilaya, ambapo kila wilaya itaunda na kusajili Umoja wake utakaojulikana kwa "Umoja wa Vijiji vyenye Hifadhi ya Misitu" (UVIHIMI). Kwa mfano, Umoja wa Vijiji vyenye Hifadhi ya Misitu Wilaya ya Kilwa (UVIHIMIKI).

Jumuiya zote zitasajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani, kila Jumuiya itakuwa na vyombo vikuu vitatu ambavyo vitakuwa na Mamlaka ya kufanya vikao vya Kikatiba kwa ajili ya kufanya maamuzi au kutoa mapendekezo kulingana na taratibu za Jumuiya. Lakini pia, taarifa hiyo ilisema Umoja wa Kitaifa wa UMJ (National CBFM Apex Body) ambao ni Chombo Kikuu cha Kitaifa cha USM utaundwa na Jumuiya zilizopata Usajili.

Mwezi Juni 2022, WWF ilifadhili mchakato wa awali wa kuanzisha Umoja wa Vijiji vyenye Hifadhi ya Misitu unaofahamika kama JUVIMIHI katika wilaya za Rufiji, Kilwa, Liwale, na Ruangwa. Mchakato huo ulisimamiwa na TAFORI kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ambapo katika kila wilaya, kikao kiliitishwa kikihusisha Wenyeviti wa KMK na Wenyeviti wa vijiji vyenye Hifadhi ya Misitu.

Malengo ya mikutano hiyo yalikuwa ni Moja, kuchagua uongozi wa Umoja na Mbili, Kuandaa rasimu ya Katiba na Kanuni ya Umoja.



Hata hivyo, mwaka 2024, FORVAC kwa kushirikiana na MCDI ilikamilisha Katiba pamoja na usajili wa jumuiya sita kama jumuiya za Kijamii (CBO) katika ngazi ya wilaya (Liwale, Ruangwa, Nachingwea, Tunduru, Namtumbo na Songea).

Kadhalika, katika hatua za ufuatiliaji wa zoezi hili Juni 25, 2025 viongozi wa kamati tendaji za UVIHIMI kutoka wilaya zote 10 walikutana katika Ukumbi wa Bandari (PTA), Mtwara, kwa lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuunda Umoja wa Kitaifa.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Maafisa Misitu na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya kutoka kila Wilaya yenye UVIHIMI isipokuwa Wilaya Kilwa. Mkutano ulifadhiliwa na WWF na uliratibiwa na wataalam kutoka TAFORI, na MCDI.

Mkutano uliazimia mambo yafuatayo: Kufanya mapitio na maboresho ya Katiba na Kanuni za UVIHIMI zilizosajiliwa kama CBO ili ziendane na matakwa ya kisheria na kukidhi vigezo vya usajili Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na Kukamilisha mchakato wa usajili wa UVIHIMI katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika, kuhakikisha utekelezaji wa maazimio hayo, mkutano uliunda Kamati ya Mpito yenye wajumbe 10, chini ya Mwenyekiti wa UVIHIMI. Kamati hii ilibuniwa kwa uwakilishi shirikishi, ambapo kila wilaya ilitoa mjumbe mmoja ili kuhakikisha usawa wa maamuzi na ushirikiano wa kitaifa katika mchakato wa uanzishwaji wa Umoja wa Kitaifa.

## Hitimisho

UVIHIMI ni jukwaa muhimu linalojumuisha vijiji vinavyotekeleza Usimamizi wa Misitu ya Jamii (UMJ). Umoja huu unalenga kuimarisha ushirikiano, uratibu, na ushawishi wa pamoja katika kulinda, kuhifadhi na kutumia kwa uendelevu rasilimali za misitu kwa manufaa ya jamii na mazingira. Sasa, kupitia UVIHIMI, vijiji vinapata nafasi ya kubadilishana uzoefu, kuimarisha sauti yao katika ngazi ya maamuzi, na kushirikiana katika kupambana na changamoto zinazovikabili katika uhifadhi wa misitu.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Umoja huu, kuna haja ya kuendelea kuimarisha juhudi za mashirika kama TAFORI, WWF na MCDI, pamoja na Serikali na wadau wengine, katika kuwezesha UVIHIMI kuwa chombo madhubuti cha usimamizi wa misitu na maendeleo endelevu ya jamii nchini Tanzania.

*Makala hii imeandaliwa na Numan Amanzi kutoka kwenye andiko la Mradi wa Ufadhili wenye jina Ushirikiano wa TAFORI, WWF na MCDI Kuimarisha Umoja wa Vijiji Vyenye Hifadhi ya Misitu Tanzania ulioandaliwa na Numan Amanzi, James Wumbura na Yuvenile Pantaleo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Shirika la Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira Duniani (WWF), Shirika la Maendeleo ya Mpingo (MCDI).*



# Conference Halls Package

**From Tsh. 200,000 - Tsh. 800,000**

Conference Hall with Air Conditioner (AC) | Stationaries | Refreshment | Bottle of Water O.5Ltrs | Internet Connection and LCD - Projector





**Tsh. 300,000**
**NSHUBEMUKI MINI CONFERENCE HALL**
1 - 15 participants per Day

**Tsh. 600,000**
**MURIRA BOARD ROOM**
1 - 35 participants per Day

**Tsh. 800,000**
**SABAS CONFERENCE HALL**
1 - 70 participants per Day

Conference Hall include; Air Conditioner (AC) | Stationaries | Refreshment | Bottle of Water 0.5Ltrs | Internet Connection and LCD - Projector

# TAFORI Conference Halls
*Packages*







**Tsh. 200,000**
**NSHUBEMUKI MINI CONFERENCE HALL**
1 - 15 participants per Day

**Tsh. 500,000**
**MURIRA BOARD ROOM**
1 - 35 participants per Day

**Tsh. 700,000**
**SABAS CONFERENCE HALL**
1 - 70 participants per Day

Conference Hall include; Air Conditioner (AC) | Stationaries | Refreshment | Bottle of Water O.5Ltrs

**CONTACTS**
0223-29-351-76 | tafori@tafori.or.tz
TAFORI HQ Morogoro, P.O.Box. 1854 | Kingolwira Highway
Morogoro - Dar es Salaam




# RESEARCHERS & PROJECT REGISTRATION

## REGISTRATION OF FORESTRY AND BEEKEEPING RESEARCHERS

### Services Requirements

Completer application form

Copy of higher education certificate

Payment receipt

Passport size photo







@taforitz | www.tafori.or.tz

# REGISTRATION PROCESS

## FEES AND OTHER CHARGES

| SN | RESEARCH ACTIVITIES | TANZANIAN RESEARCHER (TZS) | FOREIGN RESEARCHER (USD) |
|---|---|---|---|
| 1. | Researcher registration fees | 20,000 | 20 |
| 2. | Application fees for conducting research project | 20,000 | 100 |
| 3. | Registration fees for conducting research | | |
| | Student (Undergraduate) | Free | Free |
| | Student (Masters) | 30,000 | 100 |
| | Student (PhD) | 50,000 | 300 |
| | Post-Doctorate / Research fellow | 100,000 | 400 |
| | Individual Research | 200,000 | 500 |
| 4. | Extension of research | 30,000 | 100 |
| 5. | Export of specimens | 50,000 | 200 |
| 6. | Data access | 500,000 | 1000 |
| 7. | Scientific talks, lectures or seminars | 500,000 | 300 |

# REGISTRATION OF FORESTRY AND BEEKEEPING RESEARCH PROJECTS

- **Service Requirements**
- Research proposal
- Copy of the registration certificate as a researcher
- Completed application form
- Curriculum Vitae (CV)
- Signed form for adhering to procedures
- Identification letter from the Head of the Institution
- Letter from your sponsor
- Copy of Higher Education Certificate
- Payment receipt
- Passport-size photo
- Copy of NIDA identification for Tanzanians and passport for non-Tanzanians
- Name and letter of your project partner for non-Tanzanians



"Utafiti wa Misitu na Ufugaji Nyuki kwa Ustawi wa Uhifadhi na Maendeleo ya Viwanda"


**TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA - TAFORI**

Tel: +255 23 2935174 | Fax: +255 23 2935174
TAFORI HQ Morogoro, P.O.Box. 1854 | Kingolwira | Highway Morogoro - Dar es Salaam
Email: tafori@tafori.or.tz | Website: www.tafori.or.tz